**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA IRINGA**

Mkuu wa shule:- **0753-247867**
Makamu mkuu wa shule:- **0715-352575**

Shule ya Sekondari Lugalo,
S. L. P. 145,
**IRINGA.**

---

**MZAZI/MLEZI WA: ………………………………….**
**………………………………………………..**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA LUGALO KATIKA HALMASHAURI YA MANISPAA YA IRINGA, MKOA WA IRINGA MWAKA 2026**

**1. UTANGULIZI**

Awali ya yote, ninachukua fursa hii kukupongeza kwa kufaulu mtihani wako wa darasa la saba, kitendo ambacho kimekuwezesha kuchaguliwa kujiunga na shule ya sekondari ya Lugalo kuanza kidato cha kwanza mwaka 2026.

Ni matumaini yangu kwamba bahati hii utaitumia vizuri kwa juhudi na maarifa ya hali ya juu ili uweze kufanikiwa katika masomo na shughuli nyingine muhimu kama vile uzalishaji mali, michezo n.k.
Aidha ni tegemeo langu pia kuwa utakuwa na nidhamu nzuri na utatekeleza na kufuata sheria na kanuni zote za shule hii pamoja na masharti yote ya kujiunga kama yalivyo orodheshwa hapa chini.

Shule hii ni shule ya kutwa kwa kidato cha I- IV na ni mchanganyiko. Vile vile shule ina kidato cha V- VI. Kidato cha tano na cha sita ni wasichana tu na hukaa bweni. Pia kuna walemavu wa viungo na wale wa macho nao hukaa bweni.

Shule ipo mjini katika manispaa ya Iringa, kilometa mbili kutoka zilipo ofisi za Halmashauri ya Manispaa kando ya barabara iendayo Dodoma.

Shule itafunguliwa tarehe …………… unatakiwa kufika siku hiyo shule itakapofunguliwa pamoja na Mzazi/Mlezi wako ili afanye mambo yafuatayo:

a) Arudishe fomu ya ahadi ya masharti ya kujiunga na shule (F.1).
b) Arudishe fomu ya taarifa binafsi (F.2).
c) Arudishe fomu za kupimwa afya (F.3).
d) Arudishe fomu inayotoa maelekezo kuhusu matumizi ya simu shuleni (F.4).
e) Alete nakala ya cheti cha kuzaliwa.
f) Alete picha 2 za mwanafunzi za rangi (Pass port size).
g) Fomu zote hapo juu ziwekwe kwenye jalada (flat file) na kuletwa siku ya kuripoti

**NB: Usajili wa mwanafunzi utakamilika iwapo tu taarifa zote hapo juu zitawasilishwa Shuleni na**

**Mzazi/Mlezi, siku ya kuripoti. Aidha mwanafunzi hatapokelewa kama atakuja peke yake bila Mzazi/Mlezi**


Ninakutakia maandalizi mema vilevile ninakukaribisha wewe mwanafunzi na Mzazi/Mlezi hapa shuleni kwa mashauriano kuhusu ufanisi wa kazi yetu.

***KARIBU SANA LUGALO SEKONDARI***
***MOTTO: HAKUNA HAKI BILA WAJIBU***

**PRAYGOD MAKONGWA**
**MKUU WA SHULE**

## 2. MAMBO YA KUZINGATIA

### (A) SARE ZA SHULE WASICHANA





(i) Blauzi (2) nyeupe tetroni, zisizoangaza, mikono mifupi.

(ii) Sketi (2) damu ya mzee (Maroon) na tai ya rangi hiyo ya sketi. Sketi iwe ndefu ya heshima, iwe na urefu hadi kwenye kongo mbili za miguu, marinda ya kawaida ya kati (20). (Angalia picha iliyowekwa)

(iii) Jozi (2) za viatu vya ngozi vyeusi, visigino vifupi vya kufunga na kamba (unene picha inavyoonesha).

(iv) Jozi (2) za soksi nyeupe ndefu mpaka magotini.

(v) Sweta rangi ya damu ya mzee (Maroom) yenye shingo ya "V" na siyo mpasuo (hazipatikani shuleni).

(vi) Kwa wasichana wa Kiislam. Hijabu nyeupe na nusu kanzu tetroni isiyoangaza (mitandio hauruhusiwi) pamoja na sketi ndefu inayofika kwenye kongo mbili za miguu.

(vii) Nguo za michezo ni "Track suit" ya ADIDAS yenye rangi ya "Dark blue" kitambaa cha kuteleza isiyo na kofia na isiyobana mpaka kuonesha maumbo ya mwili. "T-shirt" 2 za rangi ya kijivu zenye kola isiyo na urembo au mistari zitakazovaliwa na "Track suit", jezi nyekundu au bluu na raba nyeupe au nyeusi. "Track suit" na "T-shirt" huvaliwa kila siku ya Ijumaa wakati wa mchakamchaka na jezi kiwanjani wakati wa kucheza mpira wa miguu/pete n.k.

(viii) Nguo za kushindia kwa wanafunzi wa Bweni ni (shamba dress (02) rangi ya "Dark blue" iwe ya solo ya kumwaga ndefu na ya heshima).

**TANBIHI: Mavazi yote hapo juu hayapatikani shuleni.**

### (B) SARE ZA SHULE KWA WAVULANA

i. Mashati (2) meupe tetroni, yasiyoangaza, mikono mifupi.

ii. Suruali (2) damu ya mzee (Maroon) na tai ya rangi hiyo ya suruali. Suruali iwe ndefu ya heshima, iwe na urefu hadi kwenye viatu na iwe na liseni nne na "turn up" mkunjo chini ,

iii. Jozi (2) za viatu vya ngozi vyeusi, visigino vifupi vya kufunga na kamba kama picha inavyoonesha hapo juu,sio mabuti wala raba.

iv. Jozi (2) za soksi rangi nyeusi.

v. Sweta rangi ya damu ya mzee (Maroon) yenye shingo ya "V" na siyo mpasuo.

vi. Nguo za michezo ni "Track Suit" "Dark blue" zisizobana mpaka kuonesha maumbo ya mwili. "T-shirt" 2 za rangi ya kijivu zitakazovaliwa na "Track suit", jezi nyekundu au bluu na raba nyeupe au nyeusi. "Track suit" na "T-shirt" huvaliwa kila siku ya Ijumaa wakati wa mchaka mchaka na jezi kiwanjani wakati wa kucheza mpira wa miguu/pete n.k.

**TANBIHI: Mavazi yote hapo juu hayapatikani shuleni.**

**3. MAHITAJI KWA WANAFUNZI WA BWENI**

(i) Godoro lenye ukubwa wa futi 2½ .
(ii) Mashuka mawili ya pinki na mawili meupe na foronya zake.
(iii) Blanketi 1.
(iv) Chandarua.
(v) Vyombo vya chakula (mf. Sahani, bakuli, kikombe, kijiko, n.k.).
(vi) Ndoo ndogo kwa matumizi binafsi.
(vii) Nguo za kushindia baada ya kutoka darasani (shamba dress 02) rangi ya "Dark Blue" iwe gauni ya solo ya kumwaga, ndefu ya heshima.
(viii) Sanduku dogo imara la kutunzia vitu (Tranka).
(ix) Taulo moja na kanga doti moja
(x) Mafuta ya kujipaka
(xi) Tochi
(x) Mswaki, dawa ya meno n.k.

**NB: Mabegi makubwa hayatakiwi, nafasi ndogo.**

**4. VIFAA VINGINE VYA KUMHUDUMIA MTOTO WAKO**

**(i)** Kalamu na madaftari ya masomo atakayosoma (counter book – 10 Quire 4 na daftari ndogo 10 kwa ajili ya mazoezi).
**(ii) Mwanafunzi anatakiwa kuja na bunda 1 la karatasi (REAM A4) muhula wa kwanza na bunda 1 la karatasi muhula wa pili (bunda hizi zitakabidhiwa kwenye ofisi ya makamu mkuu wa shule wakati mwanafunzi anaripoti shule**
(iii) Mzazi/Mlezi amhudumie mwanafunzi gharama za chakula cha mchana ili aweze kubaki shuleni kwa muda mrefu.
(iv) Nauli ya kwenda shuleni na kurudi nyumbani.
(v) Matibabu ya mwanao awapo mgonjwa.
**(vi) Vitabu vya kiada na ziada kwa masomo mbalimbali mf. Hisabati, Kiswahili n.k. (orodha imeambatanishwa katika kurasa za mwisho).**
(vii) Mkebe wenye vifaa vyote ndani (mathematical set).
(viii) Begi la kuwekea madaftari. N.k.
(ix) Boxing file kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu za mitihani yake nyumbani.

**5. MAMBO AMBAYO HAYARUHUSIWI SHULENI**

(i) Kuvaa vazi jingine lolote nje ya sare ya shule iwe ni soksi, viatu, sketi, sweta n.k. likivaliwa shuleni hatua za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yako.
(ii) Hereni, mikufu /shanga, kucha ndefu, kupaka kucha rangi, bangili, wanja n.k. haviruhusiwi shuleni.
(iii) Hairuhusiwi kufuga nywele, kusuka, kuziweka dawa kunyoa (kipala, panki au aina yoyote ya unyoaji) zaidi ya unyoaji uliokubalika na shule yaani nywele fupi zinazolingana kichwa chote.
(iv) Hairuhusiwi kuja na simu shuleni, ukijanayo na ukakamatwa, hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yako.

(v) Mwanafunzi wa bweni haruhusiwi kuwa na nguo za nyumbani zaidi ya sare ya shule, nguo za michezo na nguo za kushindia (Shamba dress).

(vi) Manukato makali ya aina yeyote hayaruhusiwi shuleni mf: pafyumu (mwanafunzi aje na mafuta ya kawaida ambayo hayana harufu kali).

## 6. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE KWA WANAFUNZI WOTE

Binadamu asilani kukaa pamoja si bure wana malengo. Aidha Taasisi kama hii yetu ina malengo. Ili kufanikisha malengo hayo ni lazima kuwe na kanuni na taratibu maalumu za kufuata, hususani mwanafunzi wa Lugalo sekondari anapaswa kufuata na kutekeleza kanuni na taratibu zifuatazo:

### A: MAHUDHURIO

Kuthamini muda wa kuwepo mahali unapotakiwa kwa mujibu wa ratiba au maelezo kutoka uongozi wa shule.

(i) Kuwahi kufika shuleni na kuwepo mstarini kwa muda uliopangwa ambao ni saa 1:00 asubuhi.
(ii) Kuhudhuria shuleni kwa muda wote wa masomo.
(iii) Kuhudhuria kazi zote za mikono na michezo.
(iv) Kuhudhuria mikutano ya shule (mfano baraza la shule, ukaguzi wa usafi, vikundi mbalimbali vinavyotambulika kisheria (mfano vilabu vya masomo, dini n.k)
(v) Kuitikia miito ya dharura mara moja.
(vi) Mwanafunzi anapaswa kuwepo eneo la shule wakati wote isipokuwa anapopata ruhusa maalumu kutoka kwa mwalimu husika.

### B: HESHIMA

a) Kuwathamini na kuwaheshimu wanajumuiya wote.
b) Kusimama na kumsalimu mwalimu au mtu yeyote anayekuzidi umri anapopita au kuingia mahali ulipo.
c) Kutumia lugha nzuri wakati wote.
d) Kushirikiana na kusaidiana na wanafunzi wengine katika kazi.
e) Kuthamini na kuheshimu kazi za aina zote.
f) Kuitika mara moja na kukimbilia aliko mkuu aliyekuita.
g) Kuheshimu bendera ya Taifa, picha za viongozi wa vyama na serikali, nembo ya Taifa,wimbo wa Taifa na fedha za Taifa.
h) Kuheshimu taratibu za mkutano, ofisi za shule, mali binafsi na mali ya umma.
i) Kukaa kimya darasani na kutoka kwa ruhusa ya mwalimu au kiongozi aliyepo darasani.
j) Kusimama katika mstari wakati wa kupokea huduma.
k) Kuwa mfano mzuri wa heshima na tabia njema mahali popote ulipo ndani na nje ya shule.
l) Baadhi ya tabia ambazo haziruhisiwi kwa mwanafunzi ni:
    a) Kuvuta sigara, kutumia madawa ya kulevya, pombe n.k.
    b) Kufuga kucha ndefu, ndevu, nywele ndefu/chafu.
    c) Kugombana, kutukanana, kupigana n.k.
    d) Uasherati, wizi, utapeli n.k.

### C: SARE

Unapaswa kuwa na sare za shule kwa mshono uliokubalika na kwa wakati kama ulivyopangwa.

i. Wakati wa masomo darasani.

ii. Safari zote nje ya shule kwa jina la shule.
iii. Wakati wa kwenda hospitali.
iv. Wakati wa kwenda likizo na kurudi.
v. Wakati wa maandamano.
vi. Wakati wa kwenda kwenye nyumba za ibada.
vii. Ikitokea wanafunzi wanahitaji kufika shule siku za mapumziko kama siku ya Jumamosi utatakiwa kuvaa sare iliyosahihi ya shule

**D: MIPAKA YA SHULE**

Wanafunzi wasitembelee

(a) Nyumba za Walimu na nyumba za Wafanyakazi wasio walimu bila ya kibali cha wahusika.
(b) Hairuhusiwi kabisa mwanafunzi kutembelea maeneo yafuatayo: -
  (i) Vilabu vya pombe.
  (ii) Majumba ya starehe.
  (iii) Majumba ya kufikia wageni.

**E: MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULENI**

a) Wizi.
b) Uvutaji bangi/sigara.
c) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
d) Kuoa na kuolewa wakati akiwa bado shuleni.
e) Kufanya jaribio la kujiua au kutishia kuua, kunywa sumu.
f) Uasherati, ubakaji, kushikwa ugoni/usagaji.
g) Kukutwa na simu au kifaa chochote kinachohusiana na simu kama vile: - “Betri”, “headphone”, “ line” au kasha lake n.k.
h) Kugoma na kuhamasisha mgomo.
i) Kupata mimba/kutoa mimba/kumsaidia mwenzie kutoa mimba.
j) Kupigana au kumpiga mtu yeyote yule.
k) Ulevi wa aina yoyote.
l) Kudharau wimbo na bendera ya Taifa.
m) Kusababisha mimba.
n) Utovu sugu wa nidhamu kwa ujumla.
o) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro wa muda mrefu.
p) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
q) Shule hairuhusu kusuka.
r) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria ya nchi.
s) Kushiriki au kuendeleza imani za kishirikina shuleni.
t) Kunyanyapaa au uonevu wa aina yoyote kwa mwanafunzi mwenzake.
u) Kulala nje ya shule.
v) Kugoma adhabu.

**F: MAGONJWA**

Wagonjwa wote wawapo shuleni watapata kibali cha kwenda hospitalini kupitia Ofisi ya Malezi.

**G: USAFI**

Usafi ni wajibu wa kila mwanafunzi kama sehemu muhimu ya maisha yake ya kila siku. Zingatia yafuatayo:

a) Usafi binafsi wa mwili na mavazi yake.

b) Usafi wa maeneo yafuatayo kama utakavyopangiwa; ukumbi wa chakula, ukumbi wa mikutano, mabweni, vyoo, madarasa, maabara, viwanja na barabara. Pia vyakula viliwe ndani ya bwalo la chakula tu.

**H: DINI/DHEHEBU**

(a) Shule inaruhusu kila mwanafunzi kuabudu kulingana na imani ya dini au dhehebu lake linalotambuliwa na Wazazi/Walezi wake, kwa kufuata ratiba na taratibu za shule.
(b) Mwanafunzi hataruhusiwa kubadili dini au dhehebu lake bila ya taarifa rasmi ya maandishi kutoka kwa Mzazi/Mlezi wake yaliyopitishwa na Afisa Mtendaji wake.

**J: WAGENI**

(a) Wageni hawaruhusiwi kufika shuleni kuonana na mwanafunzi wakati awapo masomoni.
(b) Wanafunzi watatembelewa na Wazazi/Walezi siku ya Jumamosi ya kila mwisho wa mwezi (wazazi/walezi watakaotambuliwa ni wale tu ambao wako kwenye jalada la mwanafunzi. Hii ni kwa wanafunzi wa bweni
(c) Taarifa za tatizo lolote lile kutoka nyumbani zitolewe kwa uongozi wa shule na siyo mwanafunzi husika moja kwa moja. Namba za simu zipo katika ukurasa wa kwanza.

**NB: Walezi/Wazazi watakao watembelea wanafunzi ni wale tu ambao taarifa zao ziko kwenye jalada la mwanafunzi (wengine hawaruhusiwi).**

**FOMU YA KUKUBALI MASHARTI YA SHULE (FOMU HII IRUDISHWE SHULENI)**

**SEHEMU YA MWANAFUNZI**

F.1

*PICHA YA MWANAFUNZI*

1. Mimi ________________________________ kidato cha ____________ ninakubali kujiunga na shule ya sekondari Lugalo nikiwa mwanafunzi wa bweni/kutwa.
2. Ninakubali masharti yote na ninaahidi kufuata sheria zote za shule.
3. Niko tayari uongozi wa shule kuchukua hatua za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kunirudisha kwa mzazi/mlezi endapo nitakiuka masharti ya shule.

Sahihi ya mwanafunzi _________________________________ Tarehe _______________

**SEHEMU YA MZAZI/MLEZI**

Mimi _____________________________________________ ninakubali mtoto wangu

kujiunga na shule ya sekondari Lugalo kuanzia tarehe ______________________,

akiwa mwanafunzi wa bweni/kutwa.

Ninakubali masharti yote yaliyomo katika maelezo ya kujiunga na shule ikiwa ni pamoja na kulipa gharama za uharibifu wa mali za umma na kumtimizia mahitaji mengine ya shule. Nitakuwa tayari kumpokea mtoto wangu wakati wowote endapo atakiuka masharti yaliyomo au kubainika kuwa ana afya isiyoridhisha ambayo itahitaji ukaribu na matunzo ya mzazi/mlezi mwenyewe.

(a) Anuani yangu ya kudumu ni:-

____________________________________________________

____________________________________________________

____________________________________________________

(b) Jina na anuani ya mlezi wa karibu mjini Iringa ambaye shule inaweza kuwasiliana naye katika matatizo mbalimbali ya mtoto ni:-

____________________________________________________

____________________________________________________

____________________________________________________

____________________________________________________

____________________________________________________

Sahihi ya mzazi/mlezi ________________________ Tarehe______________

**FOMU YA MWANAFUNZI YA KUPOKELEWA SHULENI**

F.2

1. Jina kamili la mwanafunzi ………………………………………………..………
2. Mahali ulipozaliwa …………………………………………………………………
3. Tarehe ya kuzaliwa …………………………………………………………………
4. Uraia ………………………………………………………………………..…….
5. Anwani ya nyumbani ……………………………………………...…..….
6. Anwani ya mzazi (kama tofauti na hiyo hapo juu) …………………………..…..
7. Jina la mzazi/mlezi …………………………………………………………………
8. Kazi ya mzazi/mlezi ………………………………………………………..…
9. Namba ya simu ya Mzazi/Mlezi ……………………………………………..…

**Huu ni mfano wa namna ya kujaza hapo chini**

| **Jina** | **Uhusiano** | **Anuwani** | **Simu** |
| --- | --- | --- | --- |

| Akili Mkwa | Baba | S.L.P. 145, Iringa | 0262702096 |
|---|---|---|---|
| **Jina** | **Uhusiano** | **Anwani** | **Simu** |
| **(a) ……………………..** | **………………….** | **……………………** | **…………** |
| **(b) ……………………..** | **………………….** | **……………………** | **…………** |
| **(c) ……………………..** | **………………….** | **……………………** | **…………** |
| **(d) ……………………..** | **………………….** | **……………………** | **…………** |

*PICHA YA BABA*

*PICHA YA MAMA*

**N.B:** Ndugu walioandikwa ndio wanapaswa kushughulikia masuala ya nidhamu, maendeleo na uhamisho wa mwanafunzi husika tu. Iwapo kutatokea mabadiliko kwa sababu yoyote ile, taarifa iletwe shuleni ili kufanyike mabadiliko hayo.

10. Dini **………. ……………………**
11. Kidato ulichopokelewa ………. ……………………
12. Shule uliyotoka ………. ……………………
13. Shughuli unazozipendelea mbali na masomo kama mpira wa miguu, mpira wa mikono, riadha, kuimba n.k.
14. Wilaya unayotoka ………………….. Mtaa …………………. Kata…………
15. Sahihi ya Mwanafunzi ……………………..…. Tarehe ……………………
16. Sahihi ya Mzazi ……………………………….. Tarehe ………**………**
17. Jina la Afisa Mtendaji wa kata ……………………………………………….
    Namba ya simu …………………… Sahihi ………………………………….
18. Jina la Afisa Mtendaji wa Mtaa ……………………………………………….
    Namba ya simu …………………… Sahihi ………………………………….

**SHULE YA SEKONDARI LUGALO**
**S.L.P 145, IRINGA TANZANIA**

F.3

**FOMU YA HOSPITALI**

***Fomu hii ijazwe na Mganga mkuu wa Mkoa/Wilaya na Mwanafunzi ajenayo shuleni***

Jina la Mwanafunzi ____________________________________________________

Umri ____________________________________ Jinsia ________________________

Blood Count (Red and white) _______________________________________________

Tool Examination __________________________________________________________

Urine analysis ____________________________________________________________

Syphilis Test ____________________________________________________

Eye Test ________________________________________________________

T B Test ________________________________________________________

Ears ___________________________________________________________

Chest __________________________________________________________

Spleen _________________________________________________________

Abdomen _______________________________________________________

Blood pressure ___________________________________________________

**ADDITIONAL INFORMATION** e.g. physical

______________________________________

______________________________________

______________________________________

______________________________________

I certify that the above mentioned student is fit to pursue studies

Signature ______________________________________

Designation ____________________________________

Section ________________________________________

Date __________________________________________

**NOTE:** Medical officer at the time of examination the individual for any aliments you note.

You must bring this complete form when you come to school. No pupils many enroll, without certificate of physical fitness.

**Signature**

**MAELEZO MAALUMU KUHUSU SIMU KWA KILA MWANAFUNZI** F.4

**UTANGULIZI**

Simu ni nini? Simu ni chombo cha mawasiliano kinachotumia/kupokea mawimbi ya sauti kwa njia ya kieletroniki. Simu inayokusudiwa katika maelezo haya ni simu ya mkononi ambayo inajumuisha vipuri vya simu kama vile betri, "headphone", line na kasha la simu.

**UMUHIMU WA MAWASILIANO YA SIMU**

Kwa kuwa simu inaendana na maendeleo ya sayansi na teknolojia hivyo matumizi yake kwa kiwango fulani hayaepukiki kwa takribani watu wa rika zote. Hata hivyo, matumizi ya simu kwa rika la wanafunzi yana madhara makubwa hivyo sharti yadhibitiwe ili kuleta matumizi yenye tija. Shule kwa kutambua umuhimu wa simu imeweka utaratibu rasmi wa matumizi ya simu kwa wanafunzi. Mkuu wa shule ameiteua rasmi ofisi ya malezi

kwa ajili ya kuwezesha wanafunzi kupata mawasiliano na wazazi pale inapohitajika na chini ya uangalizi maalumu. Uzoefu unaonesha kuwa wanafunzi wasiposimamiwa kikamilifu na walimu ambao wana fahamu tabia zao kwa undani wanaweza kutumia simu hizo za walezi kufanya udanganyifu na kuathiri maendeleo yao kitaaluma. Maelezo haya yanatoa angalizo kuwa ni muhimu sana matumizi ya simu yasimamiwe kikamilifu.

**ATHARI ZA MATUMIZI YA SIMU KWA WANAFUNZI**

Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa shuleni hapa kwa muda mrefu sasa, utafiti ulijaribu kuhusianisha athari za simu kwa maendeleo ya taaluma kwa wanafunzi wa kidato cha I hadi VI utafiti uling'amua athari zifuatazo: -

i. Kwa kuwa simu haziruhusiwi shuleni kwa mujibu wa kanuni na sheria za uendeshaji wa shule mwanafunzi mwenye kumiliki simu anakuwa kwenye hali ya wasiwasi wakati wote akihofu kukamatwa na simu hivyo anakosa utulivu ambao ni muhimu sana kwa mazingira ya kujifunza.

ii. Mwanafunzi mwenye simu anatumia nguvu na akili nyingi sana kutafuta sehemu ya kuficha simu, maarifa hayo yangetumika darasani yangeweza kuleta tija kubwa sana katika taaluma.

iii. Utafiti unaonyesha kuwa zaidi ya asilimia 95% ya wanafunzi wenye kumiliki simu wanazitumia simu hizo kwa ajili ya kujenga na kudumisha mahusiano ya kimapenzi na wenzao au watu wenye umri mkubwa kuliko wenyewe. Hali hii huathiri taaluma na ufaulu wa mwanafunzi kwa ujumla.

iv. Taarifa/ujumbe wa kimapenzi huwaathiri wengi kwa kuwa wanatumia muda mrefu kutafakari na kutafuta majibu yenye mshindo mkubwa ya kumrudishia mtumiaji wa awali. Vile vile ujumbe wa kimapenzi huathiri wanafunzi wengi kwa kudhani kuwa jumbe hizo ni za kweli ili hali nyingi ni za uongo na za kuwaghilibu.

v. Wanafunzi wenye kumiliki simu za mikononi hutumia muda mwingi wa usiku "kuchat" (kutumia jumbe fupi) badala ya kulala ili wapate nguvu ya kuamka asubuhi au usiku kujisomea. Hivyo wanafuzi wengi wenye simu huwa wachovu siku inayofuata, wanashindwa kumaliza kazi za nyumbani (home work) hivyo simu inachangia kurudisha nyuma maendeleo yao ya kitaaluma.

vi. Simu hurahisisha mawasiliano baina ya wanafunzi na wale wenye nia ya kuwalaghai wanafunzi wa kike kimapenzi kwa kuwa huweza kufanya ushawishi wao wakati wa usiku. Ikumbukwe kuwa wakati wa usiku mwili ukiwa umetulia hisia hutawala. Simu inaweza kumfanya mwanafunzi afikiwe na watu wasio na nia nzuri wakati wowote ule.

vii. Utafiti wetu umeng'amua kuwa simu zinasababisha wanafunzi wengi kutoroka vipindi wakati wa mchana na usiku ili wapate fursa ya kuweza kufanya mawasiliano na wenzao mbali na wanafunzi wema ambao huweza kutoa taarifa kwa walimu. Utoro wa aina hii umegunduliwa kwa wanafunzi wa kutwa wenye kutoroka vipindi wakati wa mchana na kujificha chooni ili waweze kuzungumza na rafiki zao wa kiume. Vile vile kwa upande wa bweni hufanya hivyo hivyo wakati wa mchana na usiku.

viii. Wanafunzi wengine wenye simu huzitumia simu hizo kuweka nyimbo za kusikiliza
kwa muda mrefu.

ix. Kwa kuwa wanafunzi hununua simu hizo wenyewe au hununuliwa na watu wasiokuwa wazazi wao hivyo gharama za uendeshaji simu hizo hupelekea baadhi yao kurubuniwa kirahisi au kuwa wadanganyifu kwa wazazi wao.

x. Wanafunzi wengi hutumia simu kuangalia picha za ngono, mpira na kufanya mawasiliano kwa njia za ‘Whatsup’ ‘Twitter’, ‘Face book’ ‘You tube’ n.k. mawasiliano ya aina hii huathiri sana akili zao pamoja na maendeleo yao ya kitaaluma.

**ADHABU KWA WANAFUNZI WENYE KUMILIKI SIMU**

Hivyo kwa kuzingatia madhara hayo Bodi ya Shule katika kikao chake cha tarehe 09.03.2013 iliamua kutolewa adhabu kali ikiwa ni:

Mwanafunzi atakayekutwa na kosa la kumiliki simu **au kifaa chochote cha simu kama betri, “headphone”, line au kasha lake ataadhibiwa kwa kuleta tofali ndogo 3000. Tofali hizo zitaletwa shuleni na mwanafunzi husika akiwa ameambatana na Mzazi/ mlezi wake.**

Ninaleta kwako maelezo na kiapo hiki ili lolote litakalotokea kusiwepo na lawama.

**A. MWANAFUNZI**

***KIAPO CHA KUKUBALI MAELEKEZO KUHUSU SIMU***

Mimi ___________________________________________ kidato cha ________________

Ninakubali maelekezo ya shule ya Sekondari Lugalo nikiwa mwanafunzi wa bweni/kutwa. Ninakubali masharti yote na ninaahidi kufuata utaratibu huo. Nipo tayari Uongozi wa Shule unichukulie hatua za kinidhamu ikiwemo kufukuzwa shule kama nitatenda kinyume na maelekezo haya.

**SAHIHI YA MWANAFUNZI ____________________________ TAREHE ________**

**B. MZAZI/MLEZI**

Mimi ___________________________ Mzazi/Mlezi wa _______________ wa kidato cha ______________________ nimesoma/nimesomewa na kuyaelewa maelezo yote kuhusiana na matumizi ya simu kwa mtoto wangu na nipo tayari kwa mwanangu kufukuzwa shule iwapo atapatikana na umiliki/kutumia simu bila ya uangalizi maalumu.

**SAHIHI YA MZAZI/MLEZI___________________________ TAREHE ____________**

**NB:**

- Kwa wanafunzi wa bweni; Mwanao anatakiwa kuja na sanduku la chuma dogo moja tu (tranka). Hatutampokea mwanafunzi mwenye mizigo mingine zaidi ya sanduku la chuma. Nguo za nyumbani haziruhusiwi kabisa. Endapo mwanafunzi atakutwa na nguo za nyumbani, nguo hizo zitanyang’anywa.
- Pia mwanafunzi hataruhusiwa kuja na chakula cha aina yoyote. Soda, juice, pipi, ubuyu pamoja na biskuti haviruhusiwi kabisa.
- Mwanafunzi atakayejihusisha na mapenzi shuleni ataadhibiwa kwa kuleta tofali ndogo 3,000 akiwa ameambatana na mzazi/mlezi wake.
- Mwanafunzi mwenye tabia ya utoro wa siku tatu mfululizo bila taarifa yoyote ataadhibiwa kwa kuleta tofali ndogo 1,500 akiwa ameambatana na mzazi/mlezi anayetambulika na shule.

**PRAYGOD MAKONGWA**
**MKUU WA SHULE**

## SHULE YA SEKONDARI LUGALO
## ORODHA YA VITABU VINAVYOTAKIWA KWA WANAFUNZI

**KIDATO CHA KWANZA.**

| SOMO | JINA LA KITABU | MWANDISHI |
|---|---|---|
| ENGLISH | **CLASS READERS**<br>• Mabala the Famer<br>• Hawa the Bus Driver<br>• Kalulu the Hare<br>**TEXT AND SUPPLEMENTARY BOOKS**<br>• Secondary English for Tanzania, Book 1<br>• School Certificate English, Book 1 | • Richard S. Mabala<br>• Richard S. Mabala<br>• Richard S. Mabala<br>• Oxford (OUP)<br>• Seki S.& Mwangi, W |
| KISWAHILI | • Kiswahili Kidato cha Kwanza<br>• Johari ya Kiswahili Kidato cha Kwanza | • Oxford<br>• Kyando na Wenzake |
| CHEMISTRY | • Chemistry for Secondary School Form 1 | • Oxford |
| CIVICS | • Civics for Secondary Schools, Book One Third Edition, new syllabus 2013 | • Zabron, M. Manzi |
| HISTORY | • History for Secondary Schools, Book One | • Tanzanian Institute of Education |
| BIOLOGY | • Biology for secondary schools, Book One | • Oxford |
| MATHEMATICS | • Secondary Basic Mathematics, Book One | • Tanzanian Institute of Education |
| COMPUTER | • Information and Computer Studies for Secondary Schools in Tanzania, Form One Students Book. | • Elias Maguttan, General Publishing Ltd 1ST Publisher 2007 |
| GEOGRAPHY | • Geography Course Book for Secondary Schools, Book One | • Tanzanian Institute of Education |
| PHYSICS | • Physics for You<br>• Physics for Secondary Schools, Form One | • Oxford<br>• Oxford |
| HOME ECONOMICS | • Home Science, Book One | • Jane Chege, Dorcas |

| | | |
|---|---|---|
| | | Kinathia and Muoka Kioko |

**PRAYGOD MAKONGWA.**
**MKUU WA SHULE.**